**INSTITUTE OF BIBLE AND MINISTRY**
**AICT COASTAL DIOCESE**

**MKUFUNZI: REV. DR. CLIFFORD BOONE (Cedar Crest Bible Fellowship Church)**

**19-23 NOVEMBA 2012**

1. MADA KUU: Nadharia ya uhusiano kati ya doktrini na uinjilisti.
2. LENGO KUU: Watumishi waelewe jinsi ya kuhubiri injili kulingana na doktrini ya Mungu kuwavuta watu kwa Kristo.
3. LENGO MAHUSUSI: Baada ya vipindi darasani watumishi waweze:
   a) Kuelewa hatua tatu zilizomo ndani ya mchakato wa Mungu kuwavuta watu kwa Kristo.
   b) Kuelewa umuhimu wa akili, hisia na hiari ya mtu, na jinsi ya umuhimu huu unaohusu kazi ya uinjilisti.
   c) Kuelewa wazi wajibu na lengo la mhubiri katika kila hatua.
   d) Kuchunguza kazi yao ya uinjilisti kulingana na mafundisho haya.
   e) Kusoma kitabu *Neema katika Ukombozi: kitabu cha 4*.

**UTANGULIZI**

Sisi watumishi tunabeba mzigo mzito. Tumepokea wajibu wa kuhubiri injili ili wenye dhambi watubu na kumwamini Yesu. Tunapojaribu kutimiza wajibu huu tunaona ugumu. Wengine wanasikiliza bila kuelewa. Wengine wanaelewa lakini hawataki Yesu. Wengine wanakubali ujumbe lakini haonekani kama maisha yao yamebadilika. Tena, kuna watu ambao wanasema kwamba wamemwamini Yesu lakini baada ya muda wanarudi dhambini.

Tunapoona matokeo mbalimbali na ugumu mbalimbali inatupasa kufikiri juu ya kazi yenyewe ya uinjilisti. Inatupasa kuchunguza neno la Mungu na kujiuliza, Je, kuna mafundisho gani ndani ya Biblia ambayo yanatusaidia kutenda kazi vizuri?

**Yohana 6:44** "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka."

Katika kozi hii tutachunguza Biblia kuona jinsi Mungu anavyowavuta wenye dhambi kwa Kristo. Ndipo, tutagundua jinsi wajibu wetu unaingiliana na kuvuta kwake Mungu.

Maombi yangu ni kwamba Mungu atatumia fundisho hilo kutusaidia kuelewa uinjilisti vizuri zaidi na kurudi kazini na nguvu mpya. Mungu atusaidie sote!

## KIPINDI CHA KWANZA

Kazi ya wokovu ni kazi ya Mungu. Ndani ya kazi hiyo ni wito wa Mungu, yaani Mungu kuwavuta watu kwa Yesu.

**Yohana 6:44** "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka."

**2 Timotheo 1:9** "Yeye alituokoa, akatuita tuwe watu wake yeye mwenyewe, si kwa sababu ya matendo yetu wenyewe bali kwa sababu ya kusudi lake na neema yake."

**1 Wakorintho 1:9** "Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa na yeye mwingie katika ushirika wa Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu."

Kuna hatua tatu katika mtu kuvutwa na Mungu kwa Yesu. Tuangalie hatua ya kwanza.

| KUVUTWA KWA KRISTO NA HATUA ZAKE | HATUA INATOKEA KATIKA SEHEMU GANI YA NAFSI? | NINI INATOKEA KATIKA NAFSI YA MTU? | WAJIBU NA LENGO LA MHUBIRI |
|---|---|---|---|
| 1. HATUA YA KWANZA: ________________________ | ______________ | *Mungu anawezesha akili ya mtu kuelewa _________________. *Mungu anawezesha akili ya mtu kuelewa _________________. | *Kuhubiri maelezo ya Bilia yanayohusu ___________________. *Kuhubiri maelezo ya Biblia yanayohusu ___________________. *Kulenga mtu anayesikia mahubiri _____________ _____________________ maelezo haya ya Biblia. |

Dhambi na Shetani zimeleta hali ya kipovu rohoni. Akili ya mwanadamu haiwezi kuona na kuelewa hali yake ya hatari dhambini. Pia, haiwezi kuelewa Yesu. Haiwezi kuelewa injili.

**Waefeso 4:17-18** “Basi nasema neno hili, tena nashuhudia katika Bwana, tangu sasa msienende kama Mataifa waenendavyo, katika ubatili wa nia zao; ambao akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao…”

**2 Wakorintho 4:3-4** “Maana, kama Habari Njema tunayohubiri imefichika, imefichika tu kwa wale wanaopotea. Hao hawaamini kwa sababu yule mungu wa ulimwengu huu amezitia giza akili zao wasipate kuuona wazi mwanga wa Habari Njema ya utukufu wa Kristo, ambaye ni mfano kamili wa Mungu.”

Mungu anapoanza kumvuta mtu kwa Yesu anaanza na akili ya huyu mtu. Anatia nuru akilini. Anawezesha akili ya huyu mtu kuelewa ‘ugonjwa’ wake wa dhambi na kuelewa ‘tibu’ ya Yesu. Bila kuelewa haya hawezi kumwamini. Kuelewa in lazima, tena ni hatu ya kwanza.

**Waefeso 1:17-18** “Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye; macho ya mioyo yenu yatiwe nuru…”

Inatupasa sisi watumishi kuhubiri kwa namna ya kueleza “ugonjwa’ wa dhambi na ‘tibu’ ya Yesu. Maelezo ni muhimu. Mafundisho ni sehemu kubwa ya uinjilisti.
**Waefeso 4:20-21** “Bali ninyi, sivyo mlivyojifunza Kristo; ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu.”

**SOMO:** Soma kurasa 1-10, Neema katika Ukombozi: kitabu cha 4.

**KIPINDI CHA PILI**

Dhamiri inafanya kazi muhimu ndani ya mwanadamu, lakini dhambi imeiathiri sana.

**Tito 1:15** “Kila kitu ni safi kwa watu walio safi; lakini hakuna chochote kilicho safi kwa wale waliochafuliwa na wasioamini, maana dhamiri na akili zao zimechafuliwa.”

Dhambi imeharibu zaidi ya akili ya mwanadamu. Imeathiri moyo wote pamoja na hisia. Badala ya kujiepusha na uovu na kupenda wema wenye dhambi hupenda uovu na kudharau wema. Moyo wote wa mtu unahitaji kubadalishwa na Mungu.

**Yohana 3:19** “Na hukumu yenyewe ndiyo hii: Mwanga umekuja ulimwenguni lakini watu wakapenda giza kuliko mwanga, kwani matendo yao ni maovu.”

Mungu anapovuta watu kwa Yesu anafanya kazi ndani ya akili, dhamiri, pamoja na hisia. Baada ya akili kuwezeshwa kuelewa hali halisi ya dhambi, dhamiri inafanya kazi na mtu anajiona ana hatia mbele ya Mungu. Ndipo Mungu anabadalisha hisia ya mtu na huyu mtu anajisikia vibaya kwa sababu ya dhambi zake.

**Yohana 16:8** “Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.”

**Yuda 1:15** “…ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu…”

| KUVUTWA KWA KRISTO NA HATUA ZAKE | HATUA INATOKEA KATIKA SEHEMU GANI YA NAFSI? | NINI INATOKEA KATIKA NAFSI YA MTU? | WAJIBU NA LENGO LA MHUBIRI |
|---|---|---|---|
| 2. HATUA YA PILI:<br><br>________________________ | ________________<br><br>na<br><br>________________ | *Mungu anawezesha dhamiri ya mtu<br><br>_________________.<br><br>*Mungu anawezesha hisia ya mtu<br><br>_________________<br><br>kulingana na hatia yake. | *Kuweka mafundisho ya Biblia yanayohusu dhambi juu ya msikilizaji ili ajione<br><br>___________________.<br><br>*Kuchochea ________ kulingana na dhambi na hatia.<br><br>*Kulenga mtu kuona _____________ na kujisikia ___________<br><br>kwa sababu ya dhambi yake.<br><br>. |

Inatupasa sisi watumishi kulenga dhamiri za watu na kumwomba Mungu ayatumie mahubiri yetu kuchoma mioyo ya watu.

**Matendo ya Mitume 2:37** “Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?”

**SOMO:** Soma kurasa 11-19, *Neema katika Ukombozi: kitabu cha 4*.

**KIPINDI CHA TATU**

Baada ya hisia kubadilishwa na Mungu mtu anaanza kutaka Kristo. Zamani alimchukia, lakini anapovutwa na Mungu moyo wake umegeuka na kutaka kumkaribia Yesu.

**Matendo ya Mitume 16:14** "Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu, akatusikiliza, ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana…"

Dhambi imeharibu zaidi ya akili na hisia za mwanadamu. Imeathiri moyo wote pamoja na hiari. Mtu akielewa habari ya dhambi na ya Yesu, akijisikia vibaya kwa sababu ya dhambi, akimtaka Yesu…bado hajaokoka. Hiari yake bado haijafanya uamuzi. Lazima mtu aamuru kumtegemea Yesu. Hiyo ndiyo imani. Bila hiari kuamua imani bado. Shida, lakini, ni kwamba dhambi imeharibu hiari.

**Warumi 8:5-8** "Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu."

| KUVUTWA KWA KRISTO NA HATUA ZAKE | HATUA INATOKEA KATIKA SEHEMU GANI YA NAFSI? | NINI INATOKEA KATIKA NAFSI YA MTU? | WAJIBU NA LENGO LA MHUBIRI |
|---|---|---|---|
| 3. HATUA YA TATU: ___________________ ___________________ | _______________ na _______________ | *Mungu anawezesha hisia _____________. *Hiari ____________ ndipo inaweza ___________________. * Hiari ____________ _____________Kristo. | *Kuchochea hisia kulingana na uzuri wa Kristo ili ___________________. *Kumkaribisha msikilizaji _____________________. |

Inatupasa sisi watumishi kuwakaribisha watu kumwamini Yesu. Hatuwezi kulazimisha mtu kumwamini. Hatuwezi kumwezesha kumwamini. Lakini kama Mungu anamvuta kwa Yesu basi Roho atafanya hiari yake mpya ndipo huyu mtu atamwamini Yesu. Wajibu wetu ni kumkaribisha kumwamini Yesu.

**2 Wakorintho 5:20** "Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu."

**SOMO**: Soma kurasa 19-31, *Neema katika Ukombozi: kitabu cha 4*.

## KIPINDI CHA NNE

| KUVUTWA KWA KRISTO<br><br>NA HATUA ZAKE | HATUA INATOKEA KATIKA SEHEMU GANI YA NAFSI? | NINI INATOKEA KATIKA NAFSI YA MTU? | WAJIBU NA LENGO LA MHUBIRI |
|---|---|---|---|
| 1. HATUA YA KWANZA<br><br>KUTIA NURU AKILINI | Akili | • Mungu anawezesha akili ya mtu kuelewa 'ugonjwa' wa dhambi.<br>• Mungu anawezesha akili kuelewa 'tibu' katika Kristo.<br>• Kuhubiri maelezo ya Biblia yanayohusu 'ugonjwa' wa dhambi.<br>• · Kuhubiri maelezo ya Biblia yanayohusu 'tibu' ya Kristo. | • Kulenga mtu anayesikia mahubiri aelewe na kukubali na maelezo haya ya Biblia. |
| 2. HATUA YA PILI<br><br>KUCHOMA DHAMIRI | Dhamiri<br><br>na<br><br>Hisia | • Mungu anawezesha dhamiri ya mtu kujihukumu.<br>• Mungu anawezesha hisia (mhemko) ya mtu kujisikia vibaya kulingana na hatia yake | • Kuweka mafundisho ya Biblia yanayohusu dhambi na matokeo ya dhambi juu ya msikilizaji ili ajione ana hatia mbele ya Mungu.<br>• Kuchochea hisia(au mhemko) kulingana na dhambi na hatia<br>• Kulenga mtu kuona hatia yake na kujisikia vibaya kwa sababu ya dhambi yake. |
| 3. HATUA YA TATU<br><br>KUMNENYEKEZA(KUFANYA UPYA HIARI) na IMANI | Hisia<br><br>na<br><br>Hiari | • Mungu anawezesha hisia(mhemko) kumtaka Kristo.<br>• Hiari inafanywa upya ndipo inaweza kumwamini Kristo.<br>• Hiari inaamua kumwamini Kristo.<br>• Kuchochea hisia(au mhemko) kulingana na uzuri ya Kristo ili apende kumwamini.<br>• Kutia moyo msikilizaji aendelee kukaa katika neno la Mungu na maombi. | • Kumkaribisha msikilizaji kumwamini Yesu (kumtegemea). |